JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

Juni, 2023

Dodoma



Scanned with CamScanner

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI MBAGALA.

Namba za Simu..

Mkuu wa Shule…0713516786

Makamu Mkuu wa Shule.. 0683171460

Shule ya Sekondari Mbagala

S.L.P. 46357

Dar es salaam.

Tarehe .. 15-06-2023

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……….............
S.L.P …………………………………….
…………………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MBAGALA HALMASHAURI YA TEMEKE MKOA DAR ES SALAAM MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari mbagala ipo umbali wa Kilometa 10.1 Kusini mwa manispaa ya Temeke. Usafiri wa basi kutoka mbagala zakhem unapatikana



Scanned with CamScanner

katika kituo cha mabasi zakhem Nauli ni Shilingi TSH 200 kwa mwanafunzi Shilingi TSH 500 kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 13/08/2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 14/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 30/08/2023.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi 2 za mshono Linda boksi rangi ya aggy plant au brownish purple na shati 2 nyeupe za tetron mikono mifupi kwa Wasichana.
ii. Na suruari 2 rangi aggy plant au brownish purple chini isipungue na shati nyeupe 2 za tetron mikono mifupi.
iii. Kwa wasichana wanaovaa juba ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo ni track suti ya darkblue Kwa wasichana na wavulana.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe Kwa wasichana na nyeusi Kwa wavulana .
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali Kwa wavulana.
viii. Sweta linanane na rangi ya suruari au sketi.
ix. Tai ifanane na rangi ya sketi Kwa wasichana na rangi ya suruari Kwa wavulana.
x. Tisheti zenye nembo ya Shule zitapatikana Shule I.
xi. Vesti au singlend zitakazovaliwa ndani ya shati Kwa wasichana na wavulana ziwe nyeupe.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari kubwa kaunta nane quire 4
ii. **Ream 2 za A 4 Kwa mwaka**
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa sayansi na hisabati.



Scanned with CamScanner

VIFAA VYA USAFI

| TAHASUSI | AINA YA KIFAA |
|---|---|
| CBG | reki ya chuma 1, hardbroom1, soft broom1, squeezer1, mopper na mopping basin Moja. |
| EGM | reki ya chuma 1, hardbroom1, soft broom1, squeezer1, mkasi mkubwa wa kukatia maua Moja. |
| HGE | reki ya chuma 1, hardbroom1, soft broom1, squeezer1, dawa ya kusafishia chooni aina ya LITE Lita 5. |
| HGK | reki ya chuma 1, hardbroom1, soft broom1, squeezer1, dawa ya kusafishia chooni aina ya LITE Lita 5 |
| HKL NA HGL | reki ya chuma 1, hardbroom1, soft broom1, squeezer1, sabuni ya maji Lita 5 aina ya TARMOL. |



Scanned with CamScanner

## 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Kutwa**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
viii. Kutunza mali za shule;
ix. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
x. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.



Scanned with CamScanner

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;



Scanned with CamScanner

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ……………………………….**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0713516786**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0683171460**
- **Mwandamizi Taaluma 0787149576**
- **Mwandamizi Malezi 0716233296**



Scanned with CamScanner

## FOMU YA USAJILI ( IJAZWE NA KURUDISHWA

## SHULENI) A: IJĄZWE NA MWANAFUNZI:

1. Jina kamili la mwanafunzi........................................................
2. Taifa...............................................
3. Uraia..............................................  Picha ya mwanafunzi 4. Dini..................................................

PICHA

5. Tarehe ya kuzaliwa........................................................
6. Mahali alipozaliwa................................ Wilaya................................
7. Shule ya sekondari aliyosoma..........................................................................
   ..........
8. Tarehe ya kutoka shule aliyosoma..........................................................
9. Nakala ya cheti chakuzaliwa
10. Cheti cha kumaliza kidato cha nne (Leaving certificate)
11. Nakala ya matokeo (Result slip kidato cha nne)

## B: MAELEZO BINAFSI YA MZAZI /MLEZI:

1. Jina kamili...............................................
2. Anuani kamili mjini Dar es salaam...........................
3. Sehemu unayoishi .................................................. Picha ya Mzazi/Mlezi

PICHA

4. Mtaa........................................................................................
5. Namba ya nyumba..................................................................
6. Simu ya mkononi:Baba..................................., Mama ..................................., Mlezi...............................

## C: MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/ MLEZI:

1. Jina la mwajiri na Idara..................................................................
2. Anuani yake.................................... Simu namba.........................
3. Kazi ya mzazi/ Mlezi (Meneja, Daktari, Mfanyabiashara n.k)........................

## D: SOMO LA DINI

Mimi............................................................................ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi........................................................ Kidato cha ..................................................................................................................... Ninaruhus u

mtoto wangu kuhudhuria somo ladini ya..................................Dhehebu la ..........................Siku ya Jumatano akiwa shuleni Mbagala

sekondari. Sahihi ya

Mzazi/Mlezi...............................................

Scanned with CamScanner

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA AHADI**

Mkuu wa Shule,
Mbagala Shule ya Sekondari
S.L.P 46357,
**DAR ES SALAAM**

Kwa mwanafunzi.

Mimi.......................................................................................................... ninakubali nafasi niliyopewa kuingia Kidatocha…………… mwaka ................... Katika shule ya Mbagala Sekondari.

Naahidi

kwamba:

1. Nitatii sheria zote za shule kama nilivyozisoma
2. Nitafanya bidii katika masomo na shughuli zote za shule.
3. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wowote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya shule ya Mbagala Sekondari.

**MUNGU NISAIDIE:**

Sahihi ya mwanafunzi……………………………………..
Tarehe……………………………………………

**KWA MZAZI/MLEZI:**

Mimi (Jina
Mzazi/Mlezi..........................................................................................................................................
…………

Mzazi/Mlezi
wa.......................................................................................................................................
…………

Naahidi kwamba:

1. Nitampatia mwanangu mahitaji ya shule kama yalivyotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule
2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika (maoni, adhabu) katika kumlea mwanangu
3. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani (homework) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake shuleni.
4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake.
5. Nitashirikiana na walimu kumweleza mwanangu maana ya shule na umuhimu wa kuwepo shuleni.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi……………………………. Tarehe……………………..

Scanned with CamScanner

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIAMBAGALA SECONDARY SCHOOL**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be filled by Government Medical officer and return to theHEAD OF SCHOOL Mbagala secondary school P.O. Box 46357,

A: **RE**: .......................................................

Please examine above mentioned student and comment on his/her fitness by responding to the problems below. Say Yes or No if student has health problem and if yes then STATE.

Head mistress

**Insert √ in the boxes provided**

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Hearing | Yes ☐ | No ☐ |
| ii. | Speech | Yes ☐ | No ☐ |
| iii. | Sight | Yes ☐ | No ☐ |
| iv. | Ts | Yes ☐ | No ☐ |
| v. | B.P | Yes ☐ | No ☐ |
| vi. | Diabetes | Yes ☐ | No ☐ |
| vii. | Mental Case | Yes ☐ | No ☐ |
| viii. | Physical Disability | Yes ☐ | No ☐ |

ix. Any other..................................................
..................................................................
..................................................................
..................................................................

B: Recommend if the student is fit for studentship;
..................................................................
..................................................................

C: Any other advice..............................................
..................................................................

**Name**..................

**Signature**................

**Date**..................

Scanned with CamScanner

# KIAMBATISHO CHA VITABU

- KISWAHILI 1 BY TIE
- KISWAHILI 2 BY TIE

USHAIRI

- KIMBUGA
- FUNGATE YA UHURU
- CHUNGU TAMU
- MAPENZI BORA

FASIHI

- NADHARIA YA FASIHI
- NADHARIA YA LUGHA(SARUFI)

RIWAYA 3

- MFADHILI
- VUTA NIKUVUTE
- USIKU UTAKAPOKWISHA

> TAMTHILIYA

MORANI
NGUZO MAMA
KIVULI KINAISHI
KWENYE UKINGO WA THINK

-BASIC APPLIED MATHEMATICS (TIE)

ADVANCED MATHEMATICS

- CONCEPTUAL for Secondary school Form V by P.L. MAYOMBYA
- CONCEPTUAL for Secondary school Form VI by P.L. MAYOMBYA
- ADVANCED MATHEMATICS FORM V BY TIE
- ADVANCED MATHEMATICS FORM VI BY TIE

ENGLISH LANGUAGE 1&2

1. ADVANCED LEVEL ENGLISH LANGUAGE FORM 5&6 BY SHADRACK G NDAMBO &JAMES KINUNDA
2. NOVELS.
   AMAN OF THE PEOPLE, BY CHINUA ACHEBE
   BEAUTIFUL ONES ARE NOT YET BORN by AYI KWEY ARMA
   HIS EXCELLENCY THE HEAD OF STATE By Danny Safo.
   PLAYS.
   AN ENEMY OF THE PEOPLE, BY HENRICK IBSEN

Scanned with CamScanner

I WILL MARRY WHEN I WANT by Ngugi wa thiong'o and Ngugi wa Mirrii
BETRAYAL IN THE CITY, BY FRANCIS IMBUGA
POETRY.
SELECTED POEM By Richard S Mabala

GENERAL STUDIES FOR FORM FIVE &SIX by (TIE)

BIOLOGY

BIOLOGY BIOLOGICAL SCIENCE 3RD EDITION 2011 By D.J Tayler N.P.O

- Green and G.W.Staut
- Guide to dissection by HGQ Rowlett, M.A and M.I Biology
- Dissection kit

- Four figure(mathematical table)-EGM,HE,CBG
- KAMUSI (Dictionary)
- Graph pads

ECONOMICS

ESSENTIAL FOR ADVENCED LEVEL ECONOMICS PAPER ONE. AMBROSE ODHIAMBO

- HISTORY

1. FUNDAMENTAL IN ADVENCED LEVEL FORM FIVE –SIX HISTORY ONE AND TWO BY AVELIUS T.THOBIAS (2021)
2. HOW EUROPE UNDERDEVELOPED AFRICA BY WALTER RODNEY(1972)ADVANCED HISTORY ONE
3. LEARNING ADVANCED WORLD HISTORY BY IDRISSA RAMADHANI MSUYA(2021) ONE AND TWO
4. ADVANCED LEVEL HISTORY BY SALEHE YASIN (2021) ONE AND TWO

- GEOGRAPHY
- FUNDAMENTAL GEOGRAPHY FOR ADVANCED LEVEL WRITTEN BY ADVENSUS THOBIAS
- PRACTICAL GEOGRAPHY FOR A- LEVEL BY T. I. E.
- REGIONALGEOGRAPHY FOR A-LEVEL BY T. I. E
- PHYSICAL GEOGRAPHY FOR A LEVEL BY T.I. E
- HUMAN AND ECONOMIIC GEOGRAPHY BY MSABILA. D. T

Scanned with CamScanner